*Kiswahili, Juz. 88(2), 147-164*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchunguzi wa Ikolojia-Ubeberu katika Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Nakuruto* ya Clara Momanyi

*Lina Akaka*[1]

**Ikisiri**

Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, fasihi ya Kiswahili imekuwa ikitoa mchango mkubwa kuhusu masuala ya mazingira kupitia tanzu mbalimbali za fasihi andishi na fasihi simulizi. Miongoni mwa kazi za kwanzakwanza kushughulikia suala la mazingira katika fasihi ya Kiswahili nchini Kenya ni riwaya ya Nakuruto (2009) ya Clara Momanyi. Riwaya ya Nakuruto ilitungwa wakati ambapo kazi za fasihi ya kimazingira zilikuwa haba. Makala hii inalenga kuchunguza jinsi riwaya hii inavyokosoa ubeberu dhidi ya mazingira uliofanywa na wakoloni na wenyeji. Shughuli za unyonyaji wa rasilimali za wenyeji kwa manufaa ya Wamagharibi na wenyeji zimechunguzwa pia. Riwaya ya Nakuruto iliteuliwa kimakusudi ili kuchunguza suala la ikolojia-ubeberu. Mbinu ya ukusanyaji data ya usomaji makini wa riwaya teule ilitumiwa, data ilinakiliwa na kutiwa katika mada ndogondogo. Mtafiti alinukuu madondoo yanayolenga suala la ikolojia-ubeberu katika riwaya, akayafasiri na kunukuu wanayoyasema wasomi wengine kuhusu suala hilo huku akiongozwa na Nadharia ya Uhakiki-ikolojia. Matokeo ya utafiti yalionesha bayana kwamba binadamu huyatawala na kuyaharibu mazingira kiasi cha kuhatarisha uhai katika sayari. Mwanadamu amekuwa akinyonya maliasili na kuonesha sifa za ubeberu zilizojaa choyo, ubinafsi na tamaa katika harakati yake ya kujinufaisha kutokana na maliasili ambayo inajumlisha vyanzo vya maji, milima, udongo, madini pamoja na miti.

## 1.0 Utangulizi

Ikolojia-ubeberu ni mojawapo ya mikabala ya uchunguzi wa mazingira katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Driessen (2007), ikolojia-ubeberu ni kitendo cha kuwa na mamlaka dhidi ya mazingira na unyonyaji. Mazingira ni jumla ya hali za nje, mambo na athari zinazozunguka na kuathiri kiungauhai au kundi la viungauhai (Shiva, 2012). Shiva anaendelea kufafanua kwamba, mazingira yanajumuisha ulimwengu wa asili kama vile hewa, maji, udongo, mimea, wanyama, na mtandao wa viungauhai. Suala la mazingira lilianza kupata umaarufu katika kazi za fasihi mwishoni mwa

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha na Sanaa Tendi, Shule ya Sayansi za Kijamii na Sanaa, Chuo Kikuu cha Daystar, Nairobi, Kenya.

Baruapepe: lakaka@daystar.ac.ke

karne ya 18 na mwanzoni mwa karne ya 19 baada ya mapinduzi ya viwanda barani Ulaya. Mapinduzi hayo yalisababisha maendeleo ya kiteknolojia na kuchochea uharibifu mkubwa wa mazingira ambao ulifuatiwa na mwamko wa kilongo cha mazingira (Worster, 1988). Kufuatia mapinduzi ya viwanda, Nixon (2011) anaeleza kuwa, mataifa mengi ya barani Ulaya yalipanua masilahi ya kiuchumi na kisiasa nje ya mipaka. Bara la Afrika likawa chanzo kikuu cha malighafi yaliyotumika kukuza viwanda vya Ulaya ambavyo vilihitaji malighafi kusambazwa mfululizo ili kuendeleza uzalishaji mwingi. Shughuli za kunyonya malighafi ya bara la Afrika zilianza na kusababisha uharibifu wa mazingira. Castellino (2020) anabainisha kuwa unyonyaji huo ulikiuka haki za ardhi za wenyeji na kutatiza uendelevu wa mazingira. Wasomi na wasanii walianza kuonesha wasiwasi wao dhidi ya uharibifu wa mazingira ya asili, utengaji wa binadamu na mazingira na maadili ya ulinzi wa mazingira yaliyohusiana na maendeleo ya viwanda. Vikundi mbalimbali vilianza harakati za kutetea mazingira kwa kutumia majukwaa mbalimbali kama vile ya kifasihi.

Wananadharia wa fasihi walianza kutoa wito kwa waandishi wa fasihi kubadilisha mitazamo yao kuhusu mazingira katika kazi zao. Glotfelty (1996), Buell (2009) na Mishra (2016) walipinga matumizi ya mazingira kama pambo tu la mandhari katika kazi za fasihi. Walitoa wito kwa waandishi kulichukulia suala la mazingira kwa uzito katika kazi zao. Baadhi ya mambo waliyopendekeza waandishi wayaangazie katika kazi zao ni kukosoa anthroposenia, kutumia fasihi kuhamasisha wanajamii kuhusu mazingira na kuendeleza uanaharakati wa mazingira katika fasihi licha ya kutetea haki ya mazingira. Awali, Ruekert (1978) alikuwa ameunda dhana ya uhakiki-ikolojia na kuwa mwanazuoni wa kwanza kuitumia katika insha yake ya *Literature and Ecology: An Experiment in Ecocriticism.*

Katika insha hiyo, Ruekert alipendekeza mkabala wa kiuhakiki ambao ungeunganisha fasihi na mazingira. Alijenga hoja kuwa fasihi ilikuwa na nafasi katika uhamasishaji na uelewa wa mazingira. Dhana hii haikutumiwa tena hadi mwaka 1989 ilipofufuliwa tena katika kongamano la Chama cha Fasihi ya Kimagharibi ambapo Love aliwashawishi wanafasihi kupanua mtazamo wao ili uvuke mipaka ya simulizi zilizomzingira binadamu bila kuyajali mazingira. Katika insha yake ya *Revaluing Nature: Toward an Ecological Criticism*, Love (1990) alieleza kuwa uhakiki wa kifasihi uliyatenga na kuyapuuza mazingira badala ya kutambua umuhimu wake. Hivyo, aliwataka waandishi wa fasihi kuyapa mazingira nafasi katika kazi zao. Insha ya Glotfelty (1996) ya *Ecocriticism: Literary Studies in an Age of Environmental Crisis* ndiyo iliweka msingi wa kazi kuhusu mazingira katika fasihi. Katika insha hiyo, Glotfelty alieleza uhusiano baina ya utamaduni na mazingira huku akiwashawishi wanazuoni wa fasihi kuchunguza namna simulizi zinavyowakilisha na kuunda mitazamo ya watu kuhusu ulimwengu wa asili.

Utafiti wa ikolojia ulianzia Marekani, ukapitia Ulaya na baadaye ulibisha hodi katika milango ya mabara ya Afrika na Asia (Nabeta na Ongutte, 2014). Wanaendelea kueleza kuwa, ndani ya Afrika, utafiti huo umeenea katika taasisi

nyingi za elimu ya juu nchini Afrika Kusini, mataifa ya Afrika Magharibi ya Nigeria na Ghana na sehemu ndogo ya Afrika Kaskazini. Nchini Kenya, Nabeta na Ongutte (2014) wanaeleza kuwa kilongo cha mazingira katika fasihi ya Kiswahili kilianza katika miaka ya 2000 baada ya kupenya katika taaluma za uchumi, siasa, sayansi na fasihi. Mijadala kuhusu mazingira bado inashuhudiwa katika makongamano ya kimataifa pia katika mitaala ya elimu. Suala la mabadiliko ya tabianchi lilianza kuwachochea waandishi wa fasihi kuitumia kama jukwaa la kuwahamasisha wananchi kuhusu mazingira. Fasihi ya Kiswahili ilianza kutumiwa pia kuwazindua wananchi kuhusu umuhimu wa mazingira na kufahamisha watu kuhusu athari za uharibifu wa mazingira.

Miongoni mwa kazi za fasihi ya Kiswahili zilizoandikwa kuhusu mazingira ni diwani za mashairi za *Bara Jingine* (2001) na *Rangi ya Anga* (2014), tamthilia ya *Majira ya Utasa* (2015) na riwaya za *Bustani ya Edeni* (2000), *Tikiti Maji* (2013), *Msimu wa Vipepeo* (2006) na *Nakuruto* (2009). Kazi hizi zimehakikiwa na waandishi tofautitofauti katika makala mbalimbali kwa kuchukua mikabala tofauti ya mawazo kuzihusu. Miongoni mwa kazi zilizohakikiwa ni riwaya ya *Nakuruto* (2009). Kipengele kinachohakikiwa katika makala hii ni tofauti kabisa na vipengele walivyohakiki watafiti waliotangulia. Makala hii inachunguza ubeberu uliofanywa katika mazingira ya Waafrika na wakoloni na jinsi Waafrika wenyewe walivyochangia katika ubeberu huo dhidi ya mazingira wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni.

Nabeta na Ongutte (2014) wanaeleza kuwa mwandishi wa *Nakuruto* (2009) aliwalaumu wakoloni kwa uharibifu wa mazingira barani Afrika. Katika riwaya hiyo, mwandishi ametalii hali ya mazingira katika vipindi vitatu vya kihistoria: kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Mwandishi ameonesha dhahiri namna ubeberu ulivyochangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa mazingira na baada ya mkoloni kuondoka uharibifu wa mazingira ukakithiri. Makala hii inachunguza mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuangazia suala la mazingira, hususani katika riwaya ya *Nakuruto* (2009). Suala la ubeberu uliofanyika dhidi ya mazingira barani Afrika katika kipindi cha ukoloni na baada ya kipindi cha ukoloni kama lilivyoakisiwa katika riwaya ya *Nakuruto*, ndilo linalochunguzwa katika makala hii. Baadhi ya wasomi wamehakiki kazi za fasihi za mazingira katika makala zao kama ifuatavyo.

### 1.1 Ikolojia na Fasihi

Kulingana na uchunguzi wa Mishra (2016), uhakiki-ikolojia hutumika kama mwitiko wa kifasihi na kifalsafa kwa changamoto za kimazingira ulimwenguni. Mishra anafafanua uhakiki-ikolojia kama uhusiano baina ya fasihi na mazingira huku akisisitiza nafasi yake katika kukuza uelewa wa mazingira na maadili. Mwanazuoni huyo analinganisha ikolojia inayolenga mahitaji ya binadamu na ile inayothamini mazingira. Anabainisha kuwa uhakiki-ikolojia huchochea uelewa wa mazingira, hivyo, kufanya utetezi wa mabadiliko ya mielekeo ya wanadamu kuhusu mazingira.

Mwaniki, Timammy na Ndung'u (2019) walichunguza athari za mtagusano kati ya jamii na ikolojia katika diwani za *Bara Jingine* (2001) na *Rangi ya Anga* (2014) kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhakiki-ikolojia. Miongoni mwa athari za uharibifu wa mazingira zilizobainishwa na wanazuoni hao ni uharibifu wa misitu, uharibifu wa hewa na ongezeko la joto, uchafuzi wa mito na mabwawa pamoja na mmomonyoko wa udongo. Matokeo ya uchunguzi wao yanaonesha kuwa uharibifu wa misitu, hewa, mito, mabwawa na udongo hutokana na shughuli za binadamu.

Santoso na wenzake (2020) walichunguza uhusiano kati ya binadamu na mazingira katika riwaya ya *Luka Perempuan Asap* (2017) iliyoandikwa na Nafi'ah al-Ma'rab wakiongozwa na Nadharia ya Uhakiki-ikolojia. Matokeo ya utafiti wao yalionesha kuwa uhusiano wa binadamu na mazingira katika riwaya ya *Luka Perempuan Asap* (2017) ulijumuisha uchafuzi wa hewa, majangwa, mikasa, ujenzi wa nyumba, wanyama na ardhi.

Wesonga, Ambuyo na Chimerah (2020) walichunguza nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira katika riwaya za *Tikitimaji* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Watafiti walibainisha namna mwandishi alivyotumia wahusika katika kuwasilisha maudhui ya mazingira, kueleza mitindo ya lugha iliyotumiwa kuwasilisha masuala ya mazingira na kutathmini iwapo mwandishi amefaulu kuwasilisha maudhui ya mazingira katika riwaya teule za utafiti. Nadharia za Uhakiki-ikolojia na Nadharia ya Uhalisia ziliongoza utafiti wao.

Maitaria na Mwita (2021) katika makala yao, walichunguza ubainishaji na uhifadhi wa mazingira katika methali za Kiswahili. Katika makala yao, waliainisha methali kuhusu aina za miti na maua zinazopatikana katika mazingira ya watu wa Afrika, methali kuhusu mimea ya asili, methali kuhusu nyasi, na methali kuhusu maeneo kame, madini, milima, mito, maziwa, bahari, wadudu na kadhalika. Watafiti hawa waliainisha methali za mazingira katika makundi kumi na mawili wakitoa mifano ya methali na kufasiri maana zake.

Baada ya kupitia maandiko hayo, imebainika dhahiri kuwa waandishi wa fasihi wanazidi kuonesha dharura ya kutetea mazingira kupitia kazi zao. Wanazuoni hao wamefaulu kutumia jukwaa la fasihi kuangazia namna uharibifu wa mazingira unavyoathiri uhai wa viungauhai pamoja na binadamu ulimwenguni. Miongoni mwa uharibifu huo ni ule wa misitu, hewa, mito, mabwawa na udongo kama inavyoakisiwa katika kazi zao. Isitoshe, hawaangazii tu uharibifu, bali wanawahamasisha pia watu kuhusu manufaa ya kulinda mazingira na kutoa suluhu kwa uharibifu unaoshuhudiwa katika maeneo mbalimbali.

## 1.2 Misingi ya Nadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uhakiki-ikolojia ya Glotfelty (1996). Katika makala yake ya *Ecocriticism: Literary Studies in an Age of Environmental Crisis*, alieleza kuwa fasihi ina nafasi muhimu katika kuunda na kuakisi mahusiano ya wanadamu na mazingira ya asili. Aliwahimiza waandishi wa fasihi kuondoka katika mitazamo inayozingatia tu masilahi ya binadamu katika mahusiano yake na

mazingira na kuandika kazi zinazoakisi malezi ya mazingira kwa manufaa ya wanadamu. Anasisitiza kuwa suala za mazingira siyo tu la kisayansi wala kisiasa, ni la kitamaduni na kifasihi pia. Glotfelty anatoa wito kwa wanafasihi kuingiza mitazamo ya kiikolojia katika taaluma ya fasihi na kuufanya uhakiki-ikolojia kama mkabala muhimu wa kuelewa vile simulizi zinavyoathiri mielekeo ya watu kuhusu mazingira. Kazi yake iliweka misingi ya kutambua fasihi kama chombo chenye nguvu katika mijadala kuhusu mazingira na uhamasishaji. Baadhi ya mawazo makuu kuhusu Nadharia ya Uhakiki-ikolojia aliyoyajadili ni utamaduni wa binadamu umeunganishwa na ulimwengu wa asili na fasihi inaakisi na kuathiri uhusiano huo. Alikosoa mitazamo ya kimazingira inayomuweka binadamu katikati ya kila kitu na kutoa wito wa kuwa na mitazamo inayojumuisha thamani na umuhimu wa mazingira katika kazi za fasihi.

Aidha, Glotfelty alihimiza pia fasihi itumiwe kuhamasisha wanajamii kuhusu mazingira kwa kuakisi changamoto za kiikolojia, athari za shughuli za binadamu katika mazingira na kutumia fasihi kukuza maadili ya kimazingira na uwajibikaji. Wazo kuu la Glotfelty ambalo limeongoza uchanganuzi wa riwaya teule ni la ukosoaji wa anthroposenia. Glotfelty anapinga mitazamo inayomuweka binadamu katikati ya kila kitu ambapo binadamu huyatawala na kuyanyonya mazingira bila kutambua kwamba uharibifu huo utamuangamiza. Kwa hivyo, anatetea kutambuliwa kwa thamani na umuhimu wa kila kiungauhai na mifumo ya ikolojia. Wazo la Glotfelty linalopinga anthroposenia limeteuliwa kuongoza uchanganuzi wa riwaya hii kwa sababu linaangazia namna shughuli za binadamu zinavyoathiri mazingira.

**1.3 Mbinu za Utafiti**

Mtafiti alichanganua riwaya teule kwa kutumia muundo wa utafiti wa kimaelezo. Riwaya ya *Nakuruto* ambamo data msingi ilikusanywa, ilitumika kama sampuli ya utafiti. Data za ziada zinazohusiana na masuala ya mazingira na fasihi zilikusanywa maktabani na mtandaoni. Riwaya ya *Nakuruto* iliteuliwa kimakusudi ili kuchunguzwa kwa misingi ya vipindi vya kihistoria vilivyomo. Riwaya hiyo inaakisi uharibifu wa mazingira wakati wa utawala wa wakoloni na baada ya kuondoka kwao, hivyo, inaakisi taswira dhahiri kuhusu jinsi binadamu wanavyoendeleza ubeberu dhidi ya mazingira. Data ilikusanywa kwa njia ya usomaji makini wa riwaya teule, data zinazohusiana na ubeberu dhidi ya mazingira zilinakiliwa. Mtafiti alisoma data, aliifasiri na kuiainisha katika mada ndogondogo, ambapo madondoo kutoka katika riwaya teule yalifasiriwa. Maoni ya waandishi wengine kuhusu fasiri hizo yalirejelewa na wazo la Glotfelty kuhusu anthroposenia lilirejelewa pia.

**2.0 Riwaya ya *Nakuruto* (2009)**

*Nakuruto* ni riwaya ya kinjozi, mtindo ambao hutumiwa na baadhi ya waandishi kama kiungo kati ya matukio ya kale na sasa. Ni riwaya inayoakisi ulimwengu wa kinjozi na halisi lakini ambamo ndani mna ukweli unaozingira fumbo la maisha ya kale, ya sasa na yajayo. Nakuruto ni mhusika anayebadilishabadilisha uhusika. Kuna

wakati anasawiriwa kama mkongwe na wakati mwingine kama msichana mdogo. Anatokea katika mandhari yenye utulivu, ambapo wanakijiji wana ushirikiano, wanakula na kunywa pamoja. Haya yote ni nguzo ya mshikamano. Maliasili zao zinawapa uhai, kwa mfano, mito na udongo wenye rutuba. Katika mandhari ya pili, baada ya kuja kwa wakoloni, mazingira yanabadilika. Visima vinakauka, njaa inakita mizizi, chuki na unafiki vinashamiri kinyume na hali ilivyokuwa kabla ya kuja kwa wakoloni. Baada ya mkoloni kuondoka, Waafrika wanaendeleza uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli zao za kila siku na kuchochea uanaharakati wa utetezi wa mazingira.

### 2.1 Taswira ya Mazingira ya Afrika kabla ya Kuja kwa Mkoloni

Mwandishi wa riwaya ya *Nakuruto* anachora taswira ya mazingira yalivyokuwa kabla ya kuja kwa mkoloni. Mhusika Nakuruto anapobadilika na kuwa kikongwe, anarudi nyuma katika kipindi cha kihistoria kabla ya wakoloni kuja Afrika. Katika mazungumzo yake na Nashelengai, anamwambia kuwa anawafahamu wazee wake. Anamwambia kuwa anamfahamu Magonji, baba mkwe wake, ambaye waliishi naye katika kijiji kimoja zamani. Kuhusu wakati huo, anasema:

> Hakukuwa na ukame kama siku hizi. Vyakula viligombania nafasi katika maghala na mvua zilinyesha kila wakati (uk. 14-15).

Nakuruto anatoa kauli hiyo akilinganisha mazingira yalivyokuwa zamani kabla ya mkoloni kuja barani Afrika na mazingira yalivyo sasa. Udongo ulikuwa na rutuba, Waafrika hawakutumia kemikali zilizodhuru udongo na kupunguza uzalishaji wa vyakula. Kauli kuwa vyakula viligombania nafasi katika maghala, inaonesha kuwa palikuwa na usalama wa chakula, tofauti na ilivyo sasa. Mvua ilinyesha kila wakati. Hiyo ni ishara kuwa palikuwa na miti mingi katika mazingira iliyovuta mvua. Maitaria na Mwita (2021) wanaunga mkono kauli hiyo wanaposema kuwa ukame ni baa ambalo linaweza kudhibitiwa kwa kuzingatia uhifadhi wa miti asilia na upandaji wa miti teule katika maeneo mbalimbali. Zamani kabla ya wakoloni kuja barani Afrika, miti hiyo ilikuwapo, ilimea yenyewe bila kupandwa; ndiyo maana Nakuruto anasema kuwa mvua zilinyesha kila wakati, ishara kwamba misitu ilikuwapo kwani ndio ilivuta mvua. Kuhusu suala hilo katika riwaya Nakuruto anasema:

> Kijiji hiki kilikuwa na misitu yenye aina nyingi za miti ya kiasili kama vile mivule, mipingo, mikuyu na mibambakofi. Sasa kimegeuka kuwa tambarare lililotapakaa visiki na majumba ya mafukara (uk. 108).

Kauli aliyoitoa Nakuruto inatupatia taswira ya mazingira ya kupendeza ambayo yalikuwa na aina nyingi ya miti ya asili, kisha anasikitika kuwa kijiji kimekuwa tambarare. Masikitiko ya Nakuruto yanadhihirisha uhusiano uliopo kati ya uharibifu wa misitu na upungufu wa mvua. Kwa mtazamo wa uhakiki-ikolojia, riwaya hii inaonesha jinsi shughuli za kitamaduni zinazolinda mazingira zilivyopuuzwa na badala yake tabia za unyonyaji zinazohatarisha mazingira kuendelezwa. Nakuruto

akipita katika kijiji hichohicho cha Latimbi anasikitika kuona kuwa mashamba makubwa yaliyozalisha vyakula vya asili hayakuwako tena badala yake kulikuwa na uharibifu wa mazingira uliowatumbukiza Walatimbi kwenye lindi la uchochole. Masuala kama hayo ndio yaliyomvutia Glotfelty (1996) kusema kuwa uhakiki-ikolojia hulenga kuchunguza namna fasihi inavyowakilisha uhusiano baina ya binadamu na mazingira ya asili. Uhusiano huo ni wa kibeberu unaoonyesha ubeberu wa binadamu dhidi ya mazingira. Shiva (2012) anaeleza kuwa binadamu kupitia ukoloni, ubwanyenye na sayansi ya Kimagharibi wameyatendea ubeberu mazingira ya asili. Kwa kufanya hivyo, Shiva (2021) anaeleza kuwa binadamu wanayachukulia mazingira ya asili kama kitu kisichokuwa na uhai, bali kama malighafi yanayofaa kutawaliwa, kudhibitiwa na kutumiwa. Hali hii inaakisiwa katika riwaya ya *Nakuruto,* wahusika Bw. Brooks na Ludao wanapobadilisha mikondo ya mito kwa manufaa yao, wenyeji wanapoharibu misitu ili kuchoma mkaa, na mtawala aliyetoka katika nchi ya Wanguzu anapowahamisha wenyeji ili achimbe madini kwenye ardhi yao na kupora maliasili.

Ubeberu dhidi ya mazingira ya asili katika riwaya ya *Nakuruto* unaakisi kuvunjika kwa mshikamano baina ya mazingira ya asili na binadamu. Maina, Akaka na Mavisi (2025) wanaangazia kuvunjika kwa mshikamano huo wanapojadili mikakati mbalimbali iliyowekwa na washika dau tofauti wakiwamo viongozi wa dini, mawakili, wanahabari na wanaharakati katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* kupinga uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Naye Mishra (2016) anaeleza kuwa fasihi ya Kiafrika mara nyingi huakisi mazingira ya asili si tu kama mandhari katika kazi, bali mshiriki hai katika maisha ya jamii ya kimaadili na utamaduni. Mawazo ya Mishra (2016) yanashadidiwa na Bulaya na Mhango (2019) wanaposema kuwa fasihi ni njia inayoweza kudhibiti mienendo, tabia na matendo yasiyofaa katika jamii. Wanaendelea kufafanua kuwa jamii inayokusudia kuwa na kizazi bora kinachothamini misingi ya utu, usawa, upendo na usalama wa mazingira yake, inapaswa kutilia mkazo matumizi ya fasihi ya watoto katika kufundishia mambo muhimu ya kijamii, likiwamo suala la mazingira. Isitoshe, wanamnukuu Heise (2016) anayetoa maoni kwamba fasihi ina uwezo wa kujenga utamaduni unaotakiwa kuhusu utunzaji wa mazingira wenye manufaa kwa binadamu na viumbe wengine. Nakuruto anasikitika kuhusu hali ya ukataji wa miti anayokumbana nayo vijijini pamoja na mwenendo wa maisha uliovurugika kwa kuwa alielewa kwamba hali hizo zingeyaathiri mazingira ya asili kwa njia hasi.

### 2.2.1 Ukiritimba dhidi ya Vyanzo vya Maji na Udhibiti

Castellino (2020) anaeleza kuwa dharura iliyopo ulimwenguni kuhusu hali ya anga-hewa, inahusishwa moja kwa moja na shughuli za kibepari zilizoanzishwa dhidi ya maeneo ya asili na kuendelezwa chini ya tawala za baada ya ukoloni. Halikadhalika, anafafanua kwamba shughuli hizi zilichochea mahitaji ya bidhaa, zikayafanya maeneo hayo kuwa kama chemichemi za rasilimali na kupuuza haki za wenyeji ambao walichukuliwa kama vitu na wala si binadamu. Mawazo hayo hayawahusishi

tu wakoloni katika uharibifu wa mazingira, yanawahusisha wenyeji pia. Hili linajitokeza katika riwaya ya *Nakuruto* ambapo Nakuruto alipofika katika mto Milu aliangaza macho ng'ambo ya mto na visiki vikakumbana na mboni za macho yake, uchungu ukamfuma moyoni. Nakuruto anakutana na Bw. Ludao pale ziwani alipokuwa anachimba mitaro ya kupitishia maji ya ziwa shambani mwake. Nakuruto anamwambia:

> Mmoja wao aliitwa Ludao, ambaye alikuwa akichimba mitaro ya kupitishia maji ya ziwa shambani mwake. Alikuwa amelowa jasho kutokana na kazi ile ngumu. "Mitaro mingi mnayochimba mahali hapa mtakuja kukausha Ipe Ludao." Nakuruto alitamka kwa sauti kali iliomshtua Ludao (uk. 32).

Nakuruto anamsuta Ludao kwa ukali kwa sababu ya kuchimba mitaro iliyopitisha maji ya ziwa kwenye shamba lake. Kitendo hicho kinaonesha kuwa palikuwa na ukame, ardhi ilikuwa imekauka na mvua haikuwa ikinyesha. Mambo hayo yalitokana na uharibifu wa miti ya asili ambayo ilivutia mvua zamani. Nakuruto anamuonya kuwa watakuja kulikausha ziwa Ipe kwa mitaro mingi wanayochimba. Hali kama hii inajadiliwa pia na Maitaria na Mwita (2021) wanapoeleza kuwa wanajamii hawatakiwi kutupa takataka katika mikondo ya maji kwa kuwa zinayazuia maji kutiririka inavyostahili hadi kwenye maziwa au baharini. Ludao amesawiriwa akibadilisha mkondo wa maji, jambo linalosababisha madhara ya kiikolojia. Matokeo ya shughuli za kutupa takataka kwenye mikondo ya maji na kubadilisha mkondo wa maji ni kukauka kwa maziwa au bahari. Mwaniki, Timammy na Ndung'u (2019) wanaunga mkono wazo hilo kwa kusema kuwa wanajamii wanapojishughulisha na shughuli za kilimo kando ya mito na mabwawa, wanaharibu ikolojia.

Nakuruto anajitokeza kama sauti inayotetea haki ya mazingira. Anakosoa kitendo kinachofanywa na Ludao, hivyo, kupitia kwake mwandishi anatoa mapendekezo yanayolandana na maoni ya Buell (2009) kuwa fasihi itumiwe kukosoa shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira anapotagusana nayo. Mhusika huyu anaishi katika jamii isiyotambua kuwa uhai wake unategemea kunawiri kwa mazingira. Lawama alizokuwa nazo Nakuruto dhidi ya shughuli za Ludao zinaendana na wazo la Glotfelty (1996) kuwa kazi za fasihi zitumiwe kuwahamasisha wanajamii kuhusu athari za shughuli zao kwa mazingira. Buell (2001) anaonesha namna binadamu alivyounganishwa kwa mifumo ya kiikolojia na haja ya walimwengu kubadilisha mitazamo yao ya kianthroposenia na kufikiria pia kuhusu mazingira.

Ludao anadhihirisha mtazamo wake wa kianthroposenia kutokana na shughuli yake. Mtazamo huo ni wa kibeberu, choyo na ubinafsi. Ludao ni kiwakilishi cha wanajamii wasiojali masilahi ya mazingira ya asili wala wanakijiji wengine. Ziwa Ipe likikauka kutokana na shughuli zake, atakuwa ameangamiza uhai wa viumbe wengi wa ziwa wanaolitegemea kwa uhai wao. Isitoshe, ataathiri maisha ya

wanakijiji wengi wanaotegemea ziwa hilo kwa shughuli za uvuvi, usafiri na mambo mengine.

Baada ya kutoka kwa Waipe, Nakuruto alienda hadi katika kijiji cha Walatimbi. Kijiji hicho kiliusitiri mto Milu ambao chanzo chake kilikuwa katika ziwa Nakuruto. Mto huo ulisitiriwa na ua mkubwa ulioenda masafa marefu. Katika upande mmoja wa mto, kulikuwa na eneo kubwa la shamba lililokuwa likimwagiliwa maji kutoka mtoni kwa kutumia mashine. Shamba hilo lilikuwa la Bw. Brook. Huyu ni kiwakilishi cha wakoloni waliokuja Afrika na kuanza kutumia rasilimali za asili kwa manufaa yao bila kuwajali wenyeji. Maelezo hayo hayapishani na ya Buell (2009) anayeeleza kuwa ukoloni na uharibifu wa mazingira ni mambo yanayofungamana kwa kiwango kikubwa kwa sababu, kihistoria, biashara za kikoloni ziliutumikisha ulimwengu wa asili kama rasilimali ya kunyonywa kwa ajili ya manufaa ya kibeberu. Nabeta na Ongutte (2014) wanaeleza kuwa mfumo huo hukuza uhusiano baina ya watu kuwa wa mabwana na vijakazi; na vijakazi kuwaona mabwanyenye tajiri waliomiliki njia za uzalishaji mali kama waharibifu wakuu wa mazingira. Bw. Brook aliyamiliki maji ya mto Milu, akaubinafsisha mto huo huku wanakijiji wakikosa maji na kulazimika kuyanunua kutoka katika mifereji kama anavyosema mwandishi katika dondoo lifuatalo:

> Bw. Brook aliyamiliki maji yale, akawanyima wanakijiji kuyateka kwa matumizi yao ya nyumbani. Iliwabidi Walatimbi kuyanunua kutoka katika mifereji aliyoimarisha bwanyenye huyo (uk. 38).

Mwandishi anaeleza kuwa zamani Walatimbi walimiliki maji ya mto huo waliozawadiwa na maumbile. Kauli hii inajitokeza pia katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*. Maina, Akaka na Mavisi (2025) wanaeleza kuwa Pasta Yona aliwaonesha waumini wake jinsi Bustani ya Edeni ambayo binadamu alizawadiwa na Mwenyezi Mungu ilivyoharibiwa na binadamu kwa kisingizio cha sayansi na teknolojia. Uharibifu huo wa mazingira ulisababisha maradhi kwa wanajamii. Katika riwaya ya *Nakuruto*, uhai wa wenyeji uliutegemea mto Milu lakini sasa ulidhibitiwa na bwanyenye aliyewatumikisha bila huruma. Kitendo cha kutia ua kwenye mto Milu ili kubadilisha mkondo wa maji hadi kwenye shamba lake kilikuwa hatari kwa mazingira kwa kuwa kilitishia kukauka kwa mto pamoja na ziwa Nakuruto. Wakoloni waliendeleza ubeberu dhidi ya mazingira katika nchi za Afrika kwa manufaa yao wenyewe pamoja na nchi zao na Waafrika wakarithi mienendo hiyohiyo kama ilivyojitokeza katika kisa cha Ludao (uk. 32). Wananadharia wa uhakiki-ikolojia walipinga shughuli hizi za kianthroposenia na kuhimiza waandishi wa fasihi kuitumia nadharia hii kama jukwaa la kuangazia uharibifu huo ili kuhamasisha watu kuhusu umuhimu wa mazingira ya asili kwa uhai wao na kuyatetea.

### 2.2.2 Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

Binadamu, Wamagharibi kwa Waafrika, wana nguvu dhidi ya mazingira, huyadhibiti na kuyatumia kwa manufaa yao. Hata hivyo, hawawajibiki ipasavyo katika utumiaji wa mazingira ambayo huusitiri uhai wa viumbe wote, wakiwamo wao wenyewe. Riwaya ya *Nakuruto* inaakisi hili Nakuruto anapoinuliwa na nguvu asizozifahamu kutoka katika mtaa wa akina Nashelengai. Akiwa hewani, aliuona mto uliojipinda katikati ya mbuga na misitu kwenye bonde kubwa lililokuwa na maji safi. Nakuruto aliwaona watu waliokuwa wakivua samaki lakini akaghadhabishwa na watu wengine waliokuwa wakitupa maji taka humo ziwani baada ya kufua nguo na kuoga. Nakuruto aliwaza kuwa, neema iliwashukia lakini uharibifu waliokuwa wakifanya, ndio ungekuwa chanzo cha maangamizi yao. Nakuruto anasema:

> Bwawa hili ambalo sasa ni ziwa husitiri uhai wa wanakijiji hiki kama vile mama mzazi anavyodumisha uhai wa wanawe kwa jasho lake. Lakini wasipochukua hadhari uzao wao utayeyuka mfano wa moshi katika upepo (uk. 31).

Nakuruto anaeleza kijazanda umuhimu wa bwawa kwa wanakijiji. Analilinganisha bwawa moja kwa moja na mama mzazi. Katika maisha ya kawaida, mama mzazi huwalinda wanawe kwa hali yoyote ile, na kupambana na hali zote kuhakikisha uhai wa wanawe. Aidha, bwawa hilo ni mama mzazi kwa wanakijiji ila wao kama watoto hawajatambua umuhimu wa bwawa katika maisha yao. Kauli ya Nakuruto kwamba uzao wao utayeyuka mfano wa moshi katika upepo inaonesha kuwa uharibifu wa mazingira hautaathiri tu kizazi kinachoyatumia vibaya peke yake, madhara yake yatavikabili hata vizazi vijavyo pia.

Nakuruto anapokaribia ziwa Ipe, kando ya ziwa anaona umati wa wanawake na watoto wanaofua nguo, maji taka yalikuwa yakimiminwa ziwani mfululizo, povu la sabuni lililomwagwa kwa muda wa miaka mingi liliathiri mazingira ya ziwa. Miti ya mahali hapo ilikuwa imeanza kupata manjano kwa sababu ya magadi mengi ya sabuni. Wanawake walikuwa wakiteka maji na wengine wakioga. Gugumaji lilikuwa likinyemelea taratibu likiufunika uso wa ziwa (uk. 32). Kutokana na hali aliyoishuhudia mahali hapo, Nakuruto anasema:

> Wanadamu tumetunukiwa zawadi za kudumu na Muumba lakini tunazitumia vibaya kwa hasara yetu wenyewe. Tunasafisha nyumba zetu kila siku. Miili yetu tunaisafisha kila uchao, lakini hatujali kupasafisha mahali panapositiri uhai wetu. Ole wetu, tunajikaanga kwa mafuta yetu wenyewe (uk. 33).

Maneno ya Nakuruto yanaonesha namna wanadamu wasivyoyajali mazingira, pengine kwa kutokujua kuwa ni sehemu mojawapo ya viungauhai kwa mfumo wote wa mazingira. Binadamu hujijali mwenyewe na kuyapuuza mazingira ambayo huusitiri uhai wake. Kutokana na dondoo hilo, inabainika kuwa uelewa wa mazingira wa binadamu ni finyu sana. Fasiri ya binadamu kuhusu mazingira ni ile aliyo na ukuruba nayo kama vile mwili wake na nyumba. Jambo hili linamsikitisha Nakuruto

ambaye amejitokeza kama mwanamke anayeihamasisha jamii kuhusu malezi ya mazingira na umuhimu wake kwa uhai wa viumbe wote. Kupitia kauli za Nakuruto, mwandishi anayapiga mwangwi mawazo ya Buell (2009) anayekosoa imani kwamba binadamu ndio viumbe msingi na muhimu sana ulimwenguni. Anahoji kuwa jukumu muhimu sana la wahakiki wa kimazingira ni kukosoa mwono-ulimwengu kuwa binadamu ndiye muhimu na kukuza mitazamo ya kifasihi na kitamaduni ambayo inatambua uwakala, thamani na uwepo wa viumbe visivyo binadamu. Suala la uharibifu wa mazingira limeshughulikiwa katika tanzu nyinginezo za fasihi ya Kiswahili. Mathalani, Mwaniki, Timammy na Ndung'u (2019) wanaeleza namna mtunzi wa diwani ya *Bara Jingine* (2001) alivyotumia jukwaa hilo kuwasuta wanajamii kwa uchafuzi wa bwawa la Ithanje. Wanajamii waliyachafua maji ya bwawa kwa kemikali walizozitumia katika mashamba yao yaliyokuwa kando ya bwawa hilo. Waandishi wa fasihi nchini Kenya na Afrika Mashariki kwa jumla wanatumia kazi zao kuakisi hali ya mazingira na namna watu wanavyotagusana nayo. Diwani ya *Bara Jingine* (2001) na riwaya ya *Nakuruto* zinaonesha hali sawia lakini inayotokea katika maeneo tofauti na kuakisiwa katika tanzu tofauti za fasihi.

### 2.2.3 Uchimbaji wa Madini

Barani Afrika, uchimbaji wa madini ulishika kasi chini ya utawala wa mkoloni. Baada ya miaka ya 1860, yalishuhudiwa mashindano ya kugawana Afrika kwa sababu ya rasilimali zake za madini (Pesa, 2023). Ross (2017) anaeleza kuwa ubeberu wa kiikolojia ambao uliambatana na utawala wa kikoloni wa Ulaya ulikuwa wa kiwango kikubwa sana na ukawa na athari za muda mrefu kwa mifumo ya ikolojia. Taswira hii inajitokeza katika riwaya ya *Nakuruto* pale Mzee Saluda anapomlalamikia Nakuruto namna walivyohamishwa katika ardhi zao ili kutoa nafasi kwa uchimbaji madini. Mzee Saluda anasema:

> Huyo mtawala alitoka katika nchi ya Wanguzu kisha akapita akiwaambia watu kuwa kijiji hiki kilikuwa na mgodi wa madini yenye thamani sana. Lakini madini hayangechimbwa bila kuwahamisha wanakijiji hadi kwenye ardhi nyingine ili kutoa nafasi kwa uchimbaji madini. Watu walikataa kuhamishwa. Lakini wakashawishiwa kuhama baada ya kuhadaiwa utajiri mkubwa (uk. 57).

Mtawala ambaye mzee Saluda anamrejelea hapa ni Wellingtone anayetumiwa na mwandishi kama kiwakilishi cha wakoloni waliokuja barani Afrika kunyonya madini. Kutokana na kauli za mzee Saluda katika dondoo hilo, inabainika dhahiri kuwa wakoloni walitumia uongo kuwahamisha wenyeji katika sehemu zilizokuwa na madini. Wenyeji walihamia katika ardhi kame ambako walilazimika kukata miti ili kuchoma mkaa kujikimu kwa sababu udongo ulikosa rutuba ambayo ingewawezesha kufanya shughuli za kilimo. Vitendo hivi vinaakisi ubeberu uliofanywa katika mazingira. Binadamu walitumia mazingira kwa manufaa yao bila kuweka mikakati ya kuyaendeleza. Kuhusu hili, Buell (2009) anasisitiza fasihi itumike kuonesha

umuhimu wa mazingira kwa uhai wa binadamu. Mwandishi wa riwaya ya *Nakuruto* anaakisi wazo la Buell anapoonesha uharibifu wa misitu uliofanywa na wenyeji na uchimbaji wa madini ulivyoathiri mifumo-ikolojia ya mataifa ya Afrika na kuvuruga maisha ya wenyeji. Mzee Saluda anasema:

> Basi, hapo ndipo tulihamishiwa. Wengi tulilazimika kuchoma mkaa na kwenda kuuza katika vijiji jirani ili kujinusurisha. Miti yote ikachomwa makaa. Mvua zikahama kabisa…Baada ya kumaliza miti waligeukia mchanga. Waliteka mchanga wakaukusanya mafungu na kuwauzia wajenzi wa makasri yale (uk. 57).

Katika dondoo hilo, inabainika kuwa ubeberu dhidi ya mazingira haukufanikishwa tu na mataifa ya Kimagharibi, wenyeji walichangia pia lakini kwa kulazimishwa baada ya kunyang'anywa ardhi zilizokuwa na rutuba. Huu ni mtazamo hasi dhidi ya mazingira ambapo binadamu hujali tu masilahi yao bila kufikiria kuhusu madhara ya muda mrefu wanayojiletea kwa kuharibu mazingira ya asili. Uchimbaji huo wa madini unadhihirisha ubinafsi wa mabwanyenye wa kikoloni waliowavuruga wenyeji kwenye ardhi zao. Katika harakati za kujikimu baada ya kupokonywa ardhi yenye rutuba kwa shughuli za uchimbaji wa madini, wenyeji walianza kukata miti na kuchoma mkaa ili kujikimu kimaisha. Mzee Saluda anamwambia Nakuruto kuwa Wanguzu walijenga kiwanda cha kusafisha madini hayo katika makazi ya wenyeji. Kiwanda hicho kimekuwa tishio kwa uhai wa wanakijiji. Hewa ya sumu itokayo kiwandani imesababisha vifo vya watu, wakiwamo watoto (uk. 60). Hali hii inashuhudiwa pia katika riwaya za *Tikiti Maji* na *Msimu wa Vipepeo.* Wesonga, Ambuyo na Chimerah (2020) wanaeleza kuwa hewa ya jiji ilichafuliwa na moshi wa magari yaliyotumia mafuta yenye salfa. Wamiliki wa viwanda waliposhauriwa na wanachama waliolinda mazingira kutotia salfa kwenye mafuta, walipuuza ushauri huo. Nao Maina, Akaka na Mavisi (2025) wanaeleza hali kama hiyo katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* ambapo Wanasiza waliandamana dhidi ya wamiliki wa kiwanda cha Sagasaga ili kupinga madhara yaliyotokana na moshi pamoja na maji taka yaliyotoka humo kwani viliathiri afya ya wenyeji pamoja na wafanyakazi. Kwa kuwa suala la uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda vinavyotumia rasilimali ya asili kama malighafi yake limeangaziwa katika kazi tofauti za fasihi, ni ukweli kuwa wamiliki wa viwanda huchangia kwa kiasi kikubwa katika ubeberu dhidi ya mazingira kwa shughuli zao za uharibifu.

Hilson (2020) anakosoa uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchimbaji wa madini ambao husababisha uharibifu wa udongo, uchafuzi wa maji, na kupotea kwa makazi ya viumbehai. Naye Heise (2008) anaeleza kuwa mataifa yanayoendelea kama mengi yaliyo barani Afrika huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, mataifa haya yanachangia kwa kiasi kidogo tatizo hili ikilinganishwa na mataifa tajiri yaliyo na viwanda vingi. Shughuli za binadamu ndizo zimechangia uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa. Glotfelty (1996) anasisitiza hilo kwa kusema kuwa kazi za fasihi

ziangazie masuala ya mazingira ili kuwatahadharisha walimwengu dhidi ya madhara yanayotokana na uharibifu wa mazingira.

### 2.2.4 Uharibifu wa Misitu

Misitu ni mali-asili ambayo Mungu aliwatunukia binadamu ili iendeleze uhai wao. Katika *Biblia Takatifu* (1997), kitabu cha *Mwanzo*, sura ya 2:8-15, inaelezwa kuwa Mungu alipomuumba Adamu, alimuweka kwenye shamba lililokuwa Mashariki mwa Edeni. Shambani humo mlikuwa na miti yenye matunda ya kila aina, mito, udongo wenye rutuba ambayo iliwezesha mimea kuota na kukua yenyewe bila kupandwa, chemichemi zilikuwa zinatokea ardhini na kunyunyizia mimea maji na hewa ilikuwa safi. Taswira ya mazingira katika *Biblia Takatifu* (1997) kitabu cha *Mwanzo,* sura ya 2: 8-15 inawiana na taswira ya mazingira kama yalivyosawiriwa na mwandishi wa *Nakuruto* anapoeleza:

> …msitu mkubwa ulijibainisha mbele yake. Aliweza pia kuona vilele virefu vilivyofunikwa kwa theluji...milima hiyo ilitiririsha vijito vilivyobubujikia kwenye msitu huo mkuu. Chemichemi za maji hayo zilimetameta…miti hiyo ilisheheni viumbe wa kila aina…lililomshangaza Nakuruto hakukuwa na uhasama miongoni mwa viumbe wale. Wanyama hao walilisha pamoja (kur. 4-5).

Nakuruto ana uanuwai wa uhusika. Ni mhusika anayeishi katika vipindi vitatu vya kihistoria, yaani kipindi cha kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Katika riwaya, mwandishi anaonesha hali ya mazingira katika vipindi vyote vitatu. Taswira ya mazingira kama inavyoonekana katika kurasa 4-5 ni ya kabla ya ukoloni. Kabla ya kuja kwa wakoloni, mazingira yalinawiri, Afrika ilikuwa na misitu mikubwa, milima ilikuwa na theluji, mito ilibubujika maji mengi, miti ya kila aina ilinawiri, wanyama, wadudu na ndege wa kila aina walishamiri. Udongo ulikuwa na rutuba; wakulima hawakutumia kemikali mashambani lakini walipata mazao mengi. Taswira hiyo inahitilafiana na taswira ya mazingira barani Afrika kama inavyoonekana baada ya kuja kwa wakoloni. Nakuruto kwa masikitiko anasema:

> Joto hili linalochoma ni ishara ya uharibifu wa mali asili. Ardhi iliyomilikiwa na wachache sasa imekuwa yabisi kwa kufujwa na wanyonyaji wale (uk. 53).

Uharibifu wa misitu ni suala tata linaloathiri mfumo wa ikolojia na hatimaye kuathiri mifumo ya kijamii kwa sababu misitu ni rasilimali muhimu katika mchakato mzima wa ikolojia. Suala la uharibifu wa mazingira, licha ya kuchunguzwa na wataalamu mbalimbali, limechunguzwa pia na Nabeta na Ongutte (2014) na Mwaniki, Timammy na Ndung'u (2019) na hivyo kuwa ni suala linalovuta umakini wa wahakiki na waandishi. Uharibifu wa mazingira ya Afrika ulitokana na shughuli za wakoloni walipofika kutafuta malighafi ya viwanda baada ya mapinduzi ya viwanda Ulaya.

Wakoloni waliwahamisha wenyeji kutoka katika maeneo yenye udongo wenye rutuba. Mzee Saluda anaeleza, "…hadi kwenye ardhi kame iliyojaa mawe, miamba na kokoto tupu. Sehemu isiyoweza kuzalisha chakula" (uk. 57). Wenyeji wakalazimika kuanza kukata miti ili kuchoma mkaa na kuuza ili wapate kujikimu. Pia, walichimba mchanga na kuuza. Hali hii inaonesha namna wakoloni na wenyeji walivyoshirikiana kuharibu mazingira. Hata hivyo, wenyeji waliyanyonya mazingira kutokana na hali ngumu ya maisha waliyokuwa nayo. Nakuruto mwenyewe anaonesha kuwa kitendo cha wakoloni kuwahamisha wenyeji kutoka katika makao yao ndicho kilichochea uharibifu wa mazingira miongoni mwa wenyeji. Anasema, "…majangili wale waliwasukuma katika lindi la uhitaji, mkaharibu misitu na mali asili ili kuyakimu maisha…" (uk. 71).

Shughuli za wenyeji pamoja na wakoloni zinadhihirisha ubinafsi na choyo aliyo nayo binadamu. Binadamu anaonekana kutofahamu kuwa uhai wake unategemea mazingira. Hali hii ndiyo iliyomfanya Glotfelty (1996) kusisitiza kuwa kazi za kifasihi zina uwezo wa kuakisi na kuathiri mitazamo ya watu kuhusu mazingira na kubadilisha wanavyotagusana nayo kupitia simulizi, wahusika na matukio. Alieleza kuwa fasihi inaweza kuakisi maadili ya kimazingira, uharibifu na mabadiliko. Kwa kuhakiki fasihi kwa mtazamo wa kimazingira, wasomi wangeangazia namna matini za kifasihi zinavyokosoa uharibifu wa mazingira.

Ubeberu dhidi ya mazingira unatokea katika viwango viwili. Kiwango cha kwanza ni Wamagharibi kuwahamisha wenyeji na kumiliki ardhi yao. Hatua hiyo inawasababisha wanakijiji kuharibu misitu ili kujikimu. Katika kiwango cha pili, wanakijiji wanadhihirisha nguvu zao dhidi ya mazingira wanapoharibu misitu na kuchoma mkaa. Nakuruto anasema:

> Kijiji hiki kilikuwa na misitu yenye aina nyingi za miti ya kiasili kama vile mivule, mipingo, mikuyu na mibambakofi. Sasa kimegeuka kuwa tambarare lililotapakaa visiki na vijumba vya mafukara (uk. 108).

Hali hiyo inaonesha uharibifu mkubwa uliofanywa dhidi ya misitu. Mazingira yakazorota na binadamu wakatumbukizwa kwenye lindi la uchochole. Nakuruto anayaona mazingira kama kitovu cha uhai wa wanakijiji (uk. 62) na kuyamithilisha na mama mzazi anavyoendeleza uhai wa mwanawe kupitia bubujiko la maziwa yake (uk. 51).

### 2.2.5 Udhibiti wa Ardhi

Settles (1996) anaeleza kuwa lengo la ukoloni ni kutumia rasilimali za kiuchumi, mazingira na binadamu wa mataifa yanayotawaliwa ili kuyafaidisha mataifa yanayotawala. Watawala Wazungu walifanya hilo kwa kuanzisha mfumo wa kilimo ambapo mimea ilipandwa kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya uzalishaji fedha. Settles anaendelea kufafanua kuwa ukoloni na ugawaji wa Afrika uliofanywa na watawala wa Kizungu ulitatiza ukuaji wa mifumo ya uchumi wa Waafrika.

Katika kipindi hicho cha ukoloni, biashara ya utumwa iliibuka na kuendelezwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka mia tatu (Nunn na Wantchekon, 2011). Hatimaye, serikali ya Uingereza ilipiga marufuku biashara hii (Allain, 2008). Marufuku hiyo ilifuatiwa na kipindi cha biashara halali na Afrika ikawa chanzo cha malighafi kwa viwanda vya mataifa ya bara la Ulaya ambapo kulikuwa na mapinduzi ya viwanda (Ocheni na Nwankwo, 2012). Wakoloni walianza kunyakua ardhi ya Waafrika na kupanda mimea kwa manufaa ya viwanda vya nchi zao. Katika riwaya ya *Nakuruto,* mhusika Nakuruto anasema:

> …Joto hili linalochoma ni ishara ya uharibifu wa mali-asili. Ardhi iliyomilikiwa na wachache sasa imekuwa yabisi kwa kufujwa na wanyonyaji wale (uk. 53).

Nakuruto anaendelea kusema:

> …naelewa kwamba wenyeji wake wanaishi katika ardhi kame, ardhi yabisi kama tumbo la tasa. Wamesukumwa hadi ukingoni mwa maangamizi wakaharibu udongo uliohimili uzao wao tangu azali. Nataka kuwarudishia watu hawa ardhi na utu wao… (uk. 61).

Kutokana na maneno hayo ya Nakuruto, inadhihirika kuwa wakoloni waliitumia ardhi ya Waafrika na kuharibu udongo kwa kupanda mimea iliyoyafaidisha mataifa yao. Katika riwaya ya *Nakuruto,* mwandishi anasema kuwa Bw. Brook aliwapokonya wanakijiji ardhi ili kuendeleza kilimo cha pamba. Isitoshe, aliwatumia wanakijiji kuzalisha pamba hiyo na kuisafirisha hadi nchini mwake. Hivyo ndivyo ubeberu dhidi ya ardhi ya Waafrika ulivyoendelezwa na Wazungu. Siyo Wazungu pekee walioharibu mazingira, Waafrika nao waliyaharibu. Walipohamishiwa kwenye ardhi kame na wakoloni, walilazimika kuharibu mazingira yao ili wajikimu kimaisha. Nakuruto anawaambia watu wa Maweni:

> Sikilizeni enyi watu wa Maweni…shida yenu kubwa ni maji. Majangili wale waliwasukuma katika lindi la uhitaji, mkaharibu misitu na mali asili ili kuyakimu maisha (uk. 71).

Maneno ya Nakuruto yanaonesha kuwa ubeberu dhidi ya mazingira haukuendeshwa tu na wakoloni wa Kizungu, bali Waafrika pia. Kimsingi, mazingira yamekuwa chini ya utawala wa binadamu katika jitihada zake za kujikimu kimaisha. Ubeberu dhidi ya ardhi umetokana na tamaa na ubinafsi wa baadhi ya wanadamu katika jitihada zao za kujitajirisha bila kujali masilahi ya mazingira. Mielekeo hii inakosolewa na Buell (2009) anaposema kuwa inapuuza maarifa ya kiikolojia ya wenyeji na kudhalilisha maadili ya kimazingira yasiyo ya Kimagharibi.

### 2.2.6 Upandaji wa Mimea Inayozalisha Fedha

Kabla ya kipindi cha ukoloni, jamii za Kiafrika zilikuwa na mifumo imara ya uchumi (Settles, 1996). Settles anaeleza kuwa ukomeshaji wa biashara ya utumwa ulianza mwaka 1807 serikali ya Uingereza ilipokomesha biashara hiyo miongoni mwa

mataifa iliyoyatawala. Kufuatia uamuzi huo, kipindi cha biashara halali kilianza na Afrika ikawa chanzo cha malighafi kwa mataifa ya Wazungu yaliyokuwa yakijenga viwanda kwa kasi. Malighafi yalihitajika katika viwanda hivyo. Mabwana wa kikoloni waliona haja ya kuwa na mashamba makubwa ya kuzalisha mimea kama malighafi ya viwanda hivyo. Kulikuwa na haja kubwa ya mazao ya kilimo. Afrika ndiyo ilitumiwa kuyazalisha. Wakoloni walivamia bara la Afrika na kuigawanya kwa manufaa yao wenyewe. Waliwapokonya wenyeji mashamba ili kuendeleza kilimo cha mimea inayozalisha fedha na kupata malighafi ya viwanda vyao. Riwaya ya *Nakuruto* inaakisi hali hii mwandishi anaposema:

> Bw. Brook aliwapokonya wanakijiji ardhi ili kuendeleza kilimo cha pamba…Pamba iliyochambuliwa na kusafishwa. Ilisafirishwa kwa malori nje ya kijiji na maduhuli yote yalimwendea Bw. Brook, mwenye shamba (uk. 38).

Hali kama hii ilifanya ardhi kuwa yabisi kwa sababu wingi wa mimea iliyopandwa ilinyonya virutubisho na kuiacha ardhi katika hali ya ukame. Shiva (1991) anakubaliana na wazo hilo anaposema kuwa ukulima wa pamba huchangia katika uharibifu wa udongo na kupungua kwa rutuba kwa sababu ya matumizi ya viuadudu. Muda mrefu wa upandaji wa mimea hiyo ulisababisha uharibifu wa udongo kwa kemikali za sumu zilizotumika kwenye udongo ili kuboresha mazao. Kadiri hatua hizi zilivyochukuliwa, ndivyo viungauhai vilipozidi kudhuriwa na kusababisha uharibifu wa mfumo mzima wa ikolojia. Kilimo cha mmea mmoja kwa muda mrefu, hususani mmea wa pamba, kilikosolewa pia na Bookchin (2024) akidai kuwa kilipunguza uanuwai wa viungauhai, kiliharibu udongo na kuzidisha utegemeaji wa kemikali za sumu. Bookchin (2024) anakiona kilimo cha mmea moja kama utawala wa kiikolojia, uharibifu wa udongo na unyonyaji ardhi wa kibepari.

## 3.0 Hitimisho

Uhakiki wa riwaya ya *Nakuruto* unaonesha dhahiri kuwa ubeberu dhidi ya mazingira ulianza kufanyika barani Afrika tangu wakati wa ujio wa wakoloni. Wakoloni pamoja na Waafrika walivuruga mifumo ya ikolojia. Wakoloni walivuruga jinsi Waafrika walivyokuwa wakiendesha kilimo na kuanzisha njia mpya za kilimo ambazo ziliathiri ardhi. Hali ya kiuchumi ya Waafrika baada ya kuja kwa mkoloni iliwachochea kuyaharibu mazingira katika harakati za kujikimu kimaisha. Waafrika walianza kukata miti na kuchafua mito huku wakoloni wakiyaharibu mazingira kwa kiwango kikubwa zaidi kwa shughuli zao za uchimbaji wa madini, kuvuruga mikondo ya mito na upandaji wa mimea ya kuzalisha fedha. Kutokana na masuala ya kimazingira aliyosawiri, mwandishi wa riwaya ya *Nakuruto* amedhihirisha namna fasihi inavyoweza kuchangia katika utetezi wa mazingira. Aidha, kupitia wahusika wake, ameeleza madhara yanayoweza kutokea iwapo binadamu wataendelea na shughuli zao zinazoharibu mazingira na hatimaye kuhatarisha uhai wao. Hivyo,

kupitia riwaya hii, fasihi inadhihirisha uwezo wa kujadili kisanii masuala yanayohusiana na mazingira.

**Marejeleo**

Allain, J. (2008). The Nineteenth Century Law of the Sea and the British Abolition of the Slave Trade. *The British Year Book of International Law*, *78*(1), 342. https://doi.org/:10.1093/bybil/78.1.342

Bible Society of Tanzania. (1997). *Biblia Takatifu*. Dodoma: Bible Society of Tanzania.

Bookchin, M. (2024) *Toward an Ecological Society*. Edinburgh: AK Press.

Buell, L. (2001) *Writing for an Endangered World: Literature, Culture, and Environment in the US and Beyond*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

_____ (2009) *The Future of Environmental Criticism: Environmental Crisis and Literary Imagination*. Malden, MA: Blackwell Publishing

Bulaya, J. na Mhango, P. (2019) "Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili". *Mulika*. Juz. 38: 105-125.

Driessen, P. (2007) *Eco-imperialism Green Power, Black Death*. New Delhi: Academic Foundation.

Glotfelty, C. (1996) "Ecocriticism: Literary Studies in an Age of Environmental Crisis". In *Interconnections Between Human and Ecosystem Health*. Dordrecht: Springer Netherlands. kur. 229-236.

Heise, U. K. (2008) *Sense of Place and Sense of Planet: The Environmental Imagination of the Global*. Oxford: Oxford University Press

Hilson, G. (2020) "The Africa Mining Vision: A Manifesto for more Inclusive Extractive Industry-led Development?" *Canadian Journal of Development Studies/Revue Canadienne D'études du Développement*, Juz. 41(3): 417-431. https://doi.org/10.1080/02255189.2020.1821352

Love, G. A. (1990) "Revaluing Nature: Toward an Ecological Criticism" *Western American Literature*, Juz. 25(3): 201-215. https://doi.org/10.1353/wal.1990.0079.

Maina, E., Akaka, L., na Mavisi, R. (2025). "Mikakati ya Utetezi wa Mazingira katika Riwaya za *Nakuruto* na *Bustani Ya Edeni*". *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, Juz. 3(2), 1-9. https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1105

Maitaria, J.N. na Mwita, L. C. (2021). "Methali za Kiswahili katika Ubainishaji na Uhifadhi wa Mazingira". *Katika Taaluma: Jarida la Chakita,* Juzuu (1)1: 73-81.

Mishra, S.K. (2016) "Ecocriticism: A Study of Environmental Issues in Literature". BRICS Journal of Educational Research, Juz. 6(4): 168–170.

Momanyi, C. (2009*)* *Nakuruto*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mwaniki, J., Timammy, R., na Ndung'u, M. (2019) "Athari za Mtagusano kati ya Jamii na Ekolojia Katika Ushairi wa Mberia: *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga*". *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, Juz. 1(1), 23-34. Inapatikana katika https://www.journals.eanso.org/index.php/eajss/article/view/17/10

Nabeta, S.N. na Ongutte, N.R. (2014) "Literary Enviromentalism: An Ecocritique of Kiswahili Literature". *International Journal of Ecology and Eco-solution*, Juz, 1 (2): 29-41.

Nixon, R. (2011) *Slow Violence and the Environmentalism of the Poor*. Cambridge, MA:Harvard University Press.

Nunn, N., na Wantchekon, L. (2011) "The Slave Trade and the Origins of Mistrust in Africa". *American Economic Review*, Juz. 101(7): 3221-3252. Inapatikana katika https://doi.org/10.1257/aer.101.7.3221

Ocheni, S. na Nwankwo, B.C. (2012) "Analysis of Colonialism and Its Impact in Africa". *Cross-Cultural Communication*, Juz. 8(3): 46-54. Inapatikana katika https://doi.org/10.3968/j.ccc.1923670020120803.1189

Pesa, I. (2023) "Toxic Coloniality and the Legacies of Resource Extraction in Africa". *International Review of Environmental History*, Juz. 9(2): 33-50. Inapatikana katika https://org/doi/10.3316/informit.T2024030800015801352733139

Ross, C. (2017) *Ecology and Power in the Age of Empire: Europe and the Transformation of the Tropical World*. Oxford: Oxford University Press.

Rueckert, W. (1978) Into and out of the Void: Two Essays. The Iowa Review, 62-86. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/20158874

Santoso, T., Atfalusoleh, S., Kusmanto, H., Hasjim, N., na Al-Ma'ruf, A.I. (2020) "The Relationship between Humans and Natural Environment in Luka Perempuan Asap Novel by Nafi'ah Al-Ma'rab: Literature Ecocritics Review". *International Journal of Scientific and Technology Research*, Juz. 9(1), 25-30.

Settles, J.D. (1996). "The Impact of Colonialism on African Economic Development," *Chancellor's Honors Program Projects*. Inapatikana katika https://trace.tennessee.edu/utk_chanhonoproj/182

Shiva, V. (1991) *The Violence of the Green Revolution: Third World Agriculture, Ecology and Politics*. London: Zed Books.

_______. (2012) *Making Peace with the Earth: Beyond Resource, Land and Food Wars.* London: Pluto Press.

Wesonga, E., Ambuyo, B.A. na Chimerah, R. (2020) "Nafasi ya Fasihi katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule *Tikitimaji* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006) za Wamitila, K.W. Katika *East African Journal of Swahili Studies*, Juz. 2(2): 54-64. https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.192

Worster, D. (Mh.) (1988). *The Ends of the Earth: Perspectives on Modern Environmental History*. Cambridge, MA: Cambridge University Press.